# MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA

## a) CHIMBUKO LA MFUKO

Serikali kwa kuzingatia matatizo yanayowakibili Vijana wake iliona ni vema kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao madhumuni yake makubwa ni kuwapatia Vijana Mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kuanzisha au kuimarisha miradi yao ya uzalishaji mali. Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ulianzishwa na Serikali mnamo mwaka wa fedha 1993/94 **chini ya sheria ya (The excheguer and Audit ordinance (cap. 439) no. 21 ya mwaka 1961 kifungu cha 17 kifungu kidogo cha kwanza.**

## b) LENGO LA MFUKO

Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwawezesha vijana kiuchumi kwa njia ya kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu. Mikopo hii huwasaidia Vijana mmoja mmoja au vikundi vya uzalishaji mali, kupata mitaji kwa ajili ya kuimarisha au kuanzisha miradi mipya ya kiuchumi inayowawezesha kupata kipato na hivyo kujitegemea kwa kujiajiri wenyewe. Aidha, Mfuko wa Maendeleo ya Vijana unalenga kuwajengea Vijana tabia ya kujiwekea akiba, tabia ya kukopa **kutoka** kwenye taasisi za fedha na tabia ya kutumia fedha kwa malengo yaliyokusudiwa.

## c) BAJETI YA MFUKO NA VYANZO

Bajeti ya mfuko hutokana na fedha zinazotengwa na serikali katika bajeti ya kila mwaka ambapo Vikundi vya vijana huwasilisha maandiko ya miradi yao kwa ajili ya kukopeshwa fedha zisizozidi Shilingi Milioni Kumi za kuanzisha miradi au kuendeleza miradi yao ambayo tayari imeisha anzishwa. Fedha hizi hukopeshwa kupitia SACCOS za vijana ambazo zimeanzishwa katika kila Halmashauri za Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji Tanzania Bara kwa riba ya asilimia Kumi (10%) kwa Mwaka kwa kipindi cha Miaka Miwili.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15 Wizara ilipata fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Vijana Jumla ya Shs. 2,000,000,000. Hadii kufikia Juni 30 2015 jumla ya Miradi 287 ya vijana kutoka katika Halmashauri 62 ilikuwa imepatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,637,953,520.

## d) KIWANGO CHA BAJETI KILICHOTENGWA KUFANYA TATHMINI YA MFUKO

Fedha za tathmini ya Mfuko hutokana na fedha kiasi cha Asilimia Kumi na Tano (15%) ambazo hutengwa kwa ajili ya za Uendeshaji ambapo mgawanyo wa fedha hii ni kama ifuatavyo:-

i. Ubainishaji wa Vikundi (5.5%)
ii. Uhamasishaji wa Uanzishaji SACOSS (5.5%)

iii. Kujengea Uwezo (41.5%)
iv. Ufuatiliaji na Tathmini (41.5%)
v. Uratibu na Usimamizi (6%)

Fedha hizi ni kwa ajili ya kuwezesha shughuli za Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana katika katika ngazi ya Wizara, Mikoa na Halmashauri zote ambako Mfuko huu unafanya kazi.

**e) VYANZO VYA MAPATO**

Vyanzo vya mapato ya Mfuko huu ni kutoka kwenye bajeti ya kila mwaka ya serikali kuu.

**f) ELIMU INAYOTOLEWA KWA WATU WANAONUFAIKA NA MFUKO**

Ili kufanikisha malengo ya mfuko, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri za wilaya mbalimbali zimeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujasiriamali, namna ya kuanzisha SACCOS za vijana za wilaya, uanzishaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi endelevu na jinsi ya kuwaza kimkakati. Hadi sasa mafunzo yametolewa kwenye mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Singida, Dodoma, Manyara, Kilimanjaro na Katavi.

**g) MAFANIKIO YA MFUKO**

Mafanikio kadhaa yamepatikana katika Uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kama lfuatavyo;-

- Katika Utaratibu wa awali wa Utoaji mikopo ambao ulikoma Mwezi Marchi 2013, jumla ya SACCOS 244 kutoka kwenye Halmashauri za Wilaya 121 zimepelekewa kiasi cha Tsh.5,000,000.00 kwa kila SACCOS, hivyo kufanya kiasi cha fedha zilzokopeshwa kufikia jumla ya sh, billion moja na million mia mbili na ishirini (1,220,000,000.00).
- Kutokana na Mikopo inayotolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana kutokuwa na riba kubwa na kutohitajika dhamana isiyohamishika, imewafanya Vijana wengi kukopa na hivyo kuwajengea tabia ya kukopa, kutumia mikopo kwa malengo yaliyokusudiwa na kurejesha mikopo hiyo kwa wakati hata katika taasisi nyingine za fedha.
- Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umekuwa chachu ya kuanzisha vikundi vya uzalishaji mali vya Vijana katika ngazi za Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa na kwa kiasi kikubwa kuibua fursa mpya za ajira ambazo zimepunguza umasikini miungoni mwa Vijana.

- Mfuko wa Maendeleo ya Vijana umekuwa kielelezo cha Serikali kuonyesha nia yake ya dhabiti kuhakikisha Vijana wanasaidiwa kuondokana na umasikini.

## h) CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MFUKO

- Elimu ndogo ya ujasiriamali kwa vijana walio wengi nchini. Vijana wanakabiliwa na changamoto ya kutambua uwezo wao na jinsi wanavyoweza kuutumia kubuni miradi ya uzalishaji kwa kutumia fursa zilizokaribu nao. Hali hii inasababisha Vijana wengi kukopa fedha za kuendesha miradi ambayo haitekelezeki, sio endelevu na haitengenezi ajira zenye staa kwa Vijana.
- Urejeshaji mbaya wa mikopo iliyokwisha tolewa kwa vijana .Hadi sasa kiasi cha mikopo iliyokwisha rejeshwa ni Tshs 300,000,000 kati ya Tshs.1.22 bilioni zilizokwisha tolewa katika Mpango wa awali wa Mfuko katika Mwaka wa Fedha wa 2009.
- SACCOS nyingi katika halmashauri nchini hazijajengewa uwezo wa kusimamia mikopo inayotolewa na mfuko wa vijana.
- Ukosefu wa vitendea kazi kwa maafisa ushirika katika halmashauri nchini hivyo kusababisha usimamizi mbovu wa mikopo hiyo.
- Baadhi ya Halmashauri kutorejesha katika Mfuko wa Maendeleo ya Vijana fedha za Marejesho kutoka kwa wakopaji na kuzitumia kwa matumizi mengine yasiyo stahili.